



MAANDAMANO KUELEKEA KALVARI, NA BERNARDO CAVALLINO, CHRYSLER MUSEUM OF ART

Yeye Hakugeuka

“Juu ya mlima uitwao Kalvari, wakati wafuasi wasio na msaada waki-tazama, mwili Wake wenye majeraha ulipigiliwa msalabani. Bila huruma Alifanyiwa mzaha na kulaaniwa na kubezwa. . . .

“Saa zake za maumivu zilipita wakati maisha Yake yakififia. Kutoka katika midomo Yake iliyokauka yalitoka maneno, ‘Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu: na alipokwisha kusema hayo, akakata roho.’ . . .

“Katika wakati wa mwisho, Bwana angeweza kugeuka. Lakini haku-fanya hivyo. Alipita chini ya vitu vyote ili aweze kuokoa vitu vyote. Mwili wake usio na uhai uliharakishwa lakini taratibu uliwekwa ndani ya kaburi la kuazima.”

Rais Thomas S. Monson (1927–2018), “Amefufuka!”, *Liahona*, Mei. 2010, 89.

Matumizi Binafsi: Aliteseka kutokana na maumivu makali, upweke, na kufa moyo, lakini bado Mwokozi alivumilia na kumaliza safari Yake ya maisha ya duniani kwa upendo—hata kumuomba Baba Yake kuwasamehe wale waliomsulubisha. Kwa sababu ya upendo Wake mkamilifu, tunaweza kukabiliana na majaribu na magumu yetu kwa upendo, na kwa msaada Wake tunaweza pia kuvumilia hadi mwisho.

Alikuwa ni Yeye Pekee Aliyeweza

“Kile alichofanya kingeweza tu kufanywa na Mungu. Kama Mwana Pekee wa Baba katika mwili, Yesu alirithi sifa za kiungu. Alikuwa mtu pekee aliyewahi kuzaliwa duniani ambaye ange-weza kufanya tendo hili muhimu zaidi na la kiungu. Kama Mtu pekee asiye na dhambi aliyewahi kuishi katika dunia hii, Hakuwa chini ya kifo cha kiroho. Kwa sababu ya uungu Wake, Yeye pia alikuwa na nguvu juu ya kifo cha kimwili. Hivyo Yeye alitufanyia sisi kile ambacho hatuwezi kujifanyia wenyewe. Alifungua kamba baridi za mauti Alifanya pia iwezekane kwetu kuwa na faraja ya juu na safi ya kipawa cha Roho Mtakatifu.”

Rais James E. Faust (1920–2007), Mshauri wa Pili katika Urais wa Kwanza, “Upatanisho: Tumaini Letu Kuu,” *Liahona*, Jan. 2002, 20.

Matumizi Binafsi: Kupitia Upatanisho Wake, Mwokozi alifungua kamba za kifo na alitukomboa wote kutokana na dhambi zetu ili kwamba kila mtu aweze kuwa na uzima wa milele. Yeye tu ndiye aliyekuwa na uwezo wa kutimiza kazi hiyo ya kuogofya na isiyowe-zekana. Tunapokuwa tunakabiliwa na changamoto kali, tunaweza kupata faraja katika kujua kwamba hakika Mwokozi anaweza kufanya kisichowezekana kiwezekane.



MAZISHI, NA CARL HEINRICH BLOCH